

**HOTUBA YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI
KUJITAMBULISHA KWENYE MKUTANO WA 41 WA
WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA JUMUIYA YA
MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA
LILONGWE, MALAWI, TAREHE 17 AGOSTI, 2021**

*Mheshimiwa Filipe Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji
na Mwenyekiti wa SADC;*

*Mheshimiwa Dkt. Lazarus Chakwera, Rais wa Jamhuri ya
Malawi, Mwenyeji wa Mkutano huu na Mwenyekiti
ajaye wa SADC;*

*Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali mliopo pamoja
na Wenza wenu;*

Waheshimiwa Wawakilishi wa Wakuu wa Nchi mliopo;

*Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la SADC pamoja
na Mawaziri wengine mliopo;*

Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa SADC;

Ndugu Makatibu Wakuu na Maafisa Waandamizi mliopo;

*Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi
za Kimataifa mliopo;*

Wageni Waalikwa, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana:

Ni heshima kubwa kwangu kupata fursa hii adimu na adhimu ya kuzungumza kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Leo sio mara yangu ya kwanza kuzungumza mbele ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC. Nilibahatika kuzungumza wakati wa Mkutano Maalum wa SADC uliofanyika Maputo, Msumbiji, mwezi Juni 2021; na mara kadhaa niliwahi kuzungumza mbele ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC wakati nikiwa Makamu wa Rais. Hata hivyo,

leo najitambulisha rasmi kwenu Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC nikiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kama mnavyofahamu, tarehe 17 Machi, 2021 nchi yetu iliondokewa na Kiongozi wetu mpandwa, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kwa msingi huo, naomba, kutumia fursa hii, kwa niaba ya Serikali na Watanzania wote, kutoa shukran zangu nyingi kwenu Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC kwa mshikamano mkubwa mliotuonesha wakati Taifa letu likipita kwenye kipindi kigumu katika historia yetu. Wengi wenu mlikuja kuungana nasi pale Dodoma kwenye Mazishi ya Kitaifa. Tunawashukuru sana kwa jinsi mlivyotufariji kwenye Msiba ule mkubwa. Nasi Watanzania tunatoa pole nyingi kwa viongozi wa nchi na wafanyakazi wa Sekretarieti waliotangulia

mbele za haki. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi. Amina.

Napenda pia kuwashukuru Wakuu wa Nchi na Serikali kwa jinsi mlivyonishika mkono na kunipa moyo. Kwa hakika, maneno yenu yalinipa ujasiri na kuniongezea kujiamini. Nawashukuru sana kaka zangu, kwa mshikamano na ushirikiano mkubwa mliounesha, ambao umedhihirisha kuwa sisi ni familia moja. Na kwa maana, hatuna budi kuendeleza mshikamano huu.

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali;

Napenda pia kutumia fursa hii, kuungana na wote walionitangulia kuzungumza katika kuwashukuru wenyeji wetu, Mheshimiwa Rais Chakwera, Serikali pamoja na Wananchi wa Malawi kwa mapokezi na ukarimu wao mkubwa

waliotuonesha tangu tumewasili kwenye Jiji hili la Lilongwe. Tunawapongeza pia kwa maandalizi mazuri ya Mkutano huu. Hongereni sana.

Binafsi, nimefarijika sana kutoa Hotuba yangu ya kujitambulisha hapa Malawi. Nimefurahi kwa sababu, kwa Watanzania wengi, Malawi na nyumbani; na kwa Wamalawi wengi Tanzania ni nyumbani. Kwa hiyo, hapa leo mimi nipo nyumbani. Sababu nyingine iliyonifanya nifurahi kutoa hotuba yangu ya kujitambulisha hapa Malawi ni kwamba, Malawi ndilo Taifa la kwanza kuongozwa na Rais Mwanamke kwenye eneo letu la SADC. Lakini hivi punde pia Katibu Mtendaji wa SADC ameeleza historia nyingine ya Malawi kwa wanawake. Hii inaonesha kuwa Malawi ni Taifa lenye baraka kwa wanawake. Hivyo, naamini, kwa kujitambulishia hapa,

nitaongeza msukumo kwa wanawake wengi zaidi kujiamini na kuhamasika kushiriki kwenye vyombo vya maamuzi.

Na hapa nataka kuwasihii sana kaka zangu tuzidi kushirikiana katika kuendeleza jitihada za kuwainua na kuwawezesha wanawake kwenye nchi zetu. Kwenye Mkutano wa *Generation Equality* uliofanyika hivi karibuni nchini Ufaransa, nilichaguliwa kuwa *champion* wa Masuala ya Haki za Kiuchumi za Wanawake (*Women Economic Rights and Justice*) kwenye eneo la Kusini mwa Afrika. Hivyo, nategemea Nchi Wanachama zitashirikiana na Timu yangu ya Wataalam katika kutekeleza jukumu hili.

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali;

Ni ukweli usiopingika kuwa, Jumuiya yetu imetoka mbali; na katika safari yake imepita milima na mabonde.

Mwaka jana, Jumuiya imetimiza miaka 40 tangu kuanzishwa kwake mwezi Aprili 1980. Katika kipindi hicho, mafanikio mengi makubwa yamepatikana. Sio tu kwamba nchi zetu zote sasa zipo huru, bali pia idadi ya Nchi Wanachama imeongezeka kutoka 7 hadi **16**. Aidha, Ukanda wetu unasifika kwa hali ya amani na usalama Barani Afrika. Migogoro michache iliyopo, inaendelea kushughulikiwa.

Masuala ya demokrasia, ikiwemo utaratibu wa kubadilishana uongozi, unazidi kushamiri. Na mfano mzuri ni kwenye uchaguzi uliofanyika kwa amani nchini Zambia hivi majuzi. Hali ya uchumi pia inaendelea kuimarika na biashara kati yetu inaongeza kila mwaka na hasa kutokana na kuanzishwa kwa Soko Huru mwaka 2008 na pia kuimarika

kwa miundombinu ya usafirishaji. Nawapongeza wote waliofanikisha kupatikana kwa mafanikio hayo.

Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, hatupaswi kuridhika kwa kuwa bado tunakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo kuendelea kwa hali ya umasikini, kasi ndogo ya ukuaji uchumi, tatizo la ukosefu wa ajira, magonjwa, athari za mabadiliko ya tabianchi na halikadhalika uwepo wa matishio mapya ya usalama, ikiwemo ugaidi, usambaaji wa silaha na uhalifu wa kimataifa. Changamoto nyingine zinahusu uhaba au ubovu wa miundombinu na ukosefu wa ujuzi na stadi za kazi kwa wananchi wetu. Jukumu la kutatua changamoto hizi ni letu sisi tuliopewa dhamana ya kuongoza kwa kushirikiana na wananchi wetu. Hivyo basi, hatuna budi tushirikiane.

Kwa msingi huo, nikiwa mwanachama mpya kwenye familia hii, nataka niahidi kuwa, Tanzania itaendelea kuwa mwanachama mwaminifu na mwadilifu wa Jumuiya hii. Tutaendelea kushirikiana na Nchi zote Wanachama katika kusukuma mbele ajenda ya utengamano, kushughulikia changamoto nilizozitaja na pia kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo Dira ya SADC ya Mwaka 2050; Mpango Kazi wa Maendeleo wa SADC wa Mwaka 2020 – 2030 (*Regional Indicative Strategic Development Plan*); na pia Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa SADC (*The SADC Industrialisation Strategy and Roadmap*). Kwa ujumla, Tanzania mliyoizoea itaendelea kuwa mshirika wa kutegemewa. Kama mjuavyo, Tanzania ni mionganini mwa Waasisi wa Jumuiya hii. Tumeshiriki katika kuianzisha; hivyo, tunatambua umuhimu na manufaa yake.

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali;

Mkutano huu unafanyika wakati dunia na Jumuiya yetu inaendelea kukabiliwa na Janga kubwa la ugonjwa UVIKO – 19. Mbali na kuteteresa mifumo yetu ya afya, Janga hili limekatisha uhai wa watu wengi. Na kila siku, takwimu za maambukizi mapya na vifo zinaongezeka. Njia moja kubwa ya kukabiliana na ugonjwa huu ni kuhakikisha wananchi wetu wanapata chanjo. Sisi Waswahili tuna msemo “*Kinga ni bora kuliko tiba*”. Nitumie jukwaa hili kuwashukuru wadau wetu wa afya na maendeleo kwa misaada wa chanjo wanayotupatia. Chanjo zinasaidia kupunguza maumivu na vifo.

Hata hivyo, mahitaji ya chanjo kwenye nchi zetu bado ni makubwa. Hivyo, hatuna budi kuendeleza jitihada za upatikanaji wa chanjo na pia kuzishawishi kampuni

zinazozalisha chanjo kuridhia kutoa vibali na teknolojia ili kuruhusu chanjo hizo kuzalishwa sehemu nyingine duniani ili kukidhi mahitaji yaliyopo. Aidha, nchi zetu hazina budi kushirikiana katika kujijengea uwezo sio tu wa kuzalisha chanjo lakini pia dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi na Serikali;

Janga la UVIKO-19 limeathiri pia uchumi. Takwimu za mwaka 2020 zinaonesha kushuka kwa uchumi, kupanda kwa mfumko wa bei na pia kuongezeka wastani wa Deni la Taifa kwa Pato la Taifa ukilinganisha na kiwango kilichowekwa na Kanda. Hali hii imesababisha nchi nyingi kushindwa kuhimili kulipa madeni yao ya nje. Hivyo, hatuna budi kushirikina katika kuziomba Nchi Tajiri na Taasisi za Fedha za Kimataifa kuendelea kutoa misamaha ama kurefusha muda wa ulipaji wa

madeni kwa Nchi Zinazoendelea mpaka pale Janga hili litakapopungua au kumalizika kabisa. Kuna umuhimu pia wa kuiwezesha sekta binafsi kwa kuwa nao imeathiriwa.

Sanjari na hayo, nchi zetu hazina budi kujipanga ili kunufaika na fursa zilizojitokeza katika kipindi hiki. Kama mnavyofahamu, kwenye kila changamoto kuna fursa. Na kwa msingi huo, nimefurahishwa sana na kaulimbiu ya Mkutano huu inayosema *"Bolstering Productive Capacities in the Face of COVID-19 Pandemic for Inclusive, Sustainable Economic and Industrial Transformation"*. Kaulimbiu hii inadhihirisha kuwa, licha ya mlipuko wa Janga hili, tunayo nafasi ya kukuza uchumi endapo tutaongeza uzalishaji kwenye sekta mbalimbali (viwanda, kilimo, n.k.).

Waheshimiwa Wakuu wa Nchi, Mabibi na Mabwana;

Nimepewa fursa ya kusalimia na kujitambulisha. Mengi tutaendelea kujadiliana kwenye mikutano yetu na wakati tutapokuwa tukitembeleana. Kwa hiyo, ninapoelekea kuhitimisha salamu zangu, napenda niungane na wote walionitangulia kuzungumza kumpongeza Mwenyekiti anayemaliza muda wake, Kaka yangu, Mheshimiwa Rais Filipe Nyusi wa Msumbiji kwa kazi kubwa na nzuri ya kuongoza Jumuiya yetu katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita; licha ya changamoto ya mlimpuko wa UVIKO - 19.

Nampongeza pia kaka yangu, Mheshimiwa Rais Dkt. Lazarus Chakwera wa Malawi kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti Mpya wa Jumuiya yetu. Halikadhalika, nampongeza Mgeni mwenzangu, Mheshimiwa Rais Wavel Ramkalawan wa Shelisheli kwa kuaminiwa na wananchi kuwa

Kiongozi wa Taifa hilo. Kwa pamoja nyote, nawaahidi ushirikiano mkubwa.

Nihitimishe kwa kuishukuru na kuipongeza Sekretarieti ya SADC kwa maandalizi mazuri ya Mkutano huo. Kwa namna ya pekee, namshukuru na kumpongeza sana Katibu Mtendaji wa SADC, ambaye anamaliza muda wake, Dkt. Stergomena Taxi, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Jumuiya yetu kwa kipindi cha miaka 8 iliyopita; licha ya changamoto nyingi zilizojitokeza. Tanzania inakushukuru na kukupongeza kwa kutuwakilisha vyema na kulinda heshima tuliyopewa na wenzetu; na tunakutakia kila la heri katika majukumu mengine utakayopangiwa. Na katika hilo, nataka kuarifu hadhira hii kuwa, tayari nimemshampangia majukumu mengine Dkt. Tax;

hivyo atakaporejea tu, ataenda kuanza kuyatumikia. Tunataka kuendelea kutumia maarifa, ujuzi na uzoefu alioupata.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, namwahidi Katibu Mtendaji mpya atakayechaguliwa; kuwa tutampa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake ya kusukuma mbele gurudumu la maendeleo kwenye Jumuiya yetu.

Baada ya kusema hayo:

Mungu Ibariki Jumuiya yetu!

Muito Obrigado!

Merci Beaucoup!

Thank You Very Much!

Zikomo Kwambiri!

“AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA”